# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

## KIKAO CHA HAMSINI NA TATU

**19 JUNI, 2026**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA TATU

### KIKAO CHA HAMSINI NA TATU – TAREHE 19 JUNI, 2026

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA:**

Hati ya Uhamisho wa Bajeti Baina ya Mafungu Na. 1 kwa Mwaka 2025/2026 *[Statement of Reallocation Between Votes - Reallocation Statement No. 1 of 2025/2026]*; na

Hati ya Uhamisho wa Bajeti Ndani ya Mafungu Na. 2 kwa Mwaka 2025/2026 *[Statement of Reallocation Within Votes - Reallocation Statement No. 2 of 2025/2026].*

**III. MASWALI:**

**OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):**

**630. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itafungua njia mpya ya Irikaswa kuelekea Mlima Kilimanjaro.

**631. MHESHIMIWA DOUGRAS DIDAS MASSABURI (KIVULE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Banana - Kitunda - Kivule hadi Mbondole Msongola kwa Kiwango cha lami.

**632. MHESHIMIWA ANNE KILANGO MALECELA (SAME MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga Kituo cha Afya Kata ya Maore kwa kuwa ina watu takribani 19,129.

**WIZARA YA KILIMO:**

**633. MHESHIMIWA KANGI ALPHAXARD LUGOLA (MWIBARA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Mradi wa Umwagiliaji wa Kasuguti utakamilika.

**634. MHESHIMIWA ENG. CHACHA MWITA WAMBURA (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji katika Jimbo la Geita Mjini ili kuongeza tija ya uzalishaji wa Kilimo.

**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:**

**635. MHESHIMIWA MARTHA FESTO MARIKI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuondoa changamoto ya Watoto wa mtaani.

**WIZARA YA AFYA:**

**636. MHESHIMIWA KASSIM HASSAN HAJI (MWANAKWEREKWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali imejipangaje kuboresha Vifaa Tiba na rasilimali watu ili kuongeza ufanisi wa huduma kwa Wananchi wanaotumia Bima ya Afya hasa Vijijini.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**637. MHESHIMIWA KHALID MUSSA NSEKELA (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:-

Je, lini Masoko ya Nkwenda na Murongo yataboreshwa ili Wakulima na Wafanyabiashara wapate masoko na kukuza biashara za mpakani.

**WIZARA YA UJENZI:**

**638. MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (SONGEA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya Lumecha - Londo - Malinyi ili kuunganisha Mkoa wa Ruvuma na Morogoro.

**WIZARA YA NISHATI:**

**639. MHESHIMIWA JESCA DAVID KISHOA (IRAMBA MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, Mkataba baina ya Serikali na Kampuni ya Songas umeongezwa au umevunjwa.

**640. MHESHIMIWA BENJAMIN LUKUBHA NGAYIWA (KAHAMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Serikali itawaunganishia umeme kwa bei ya REA badala ya TANESCO Wananchi wa baadhi ya maeneo ya Vijiji yaliyotambulika kama Miji - Kahama.

## WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**641. MHESHIMIWA DICKSON NATHAN LUTEVELE (MAFINGA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Soko kubwa la mazao ya misitu ili Wanunuzi wa kigeni wasiende kununua moja kwa moja kwa Wakulima Vijijini.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UWEKEZAJI):**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2025 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

***(Majadiliano yanaendelea)***

| | |
|---|---|
| **DODOMA** | **BARAKA I. LEONARD** |
| **19 JUNI, 2026** | **KATIBU WA BUNGE** |